

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA**

MKOZA WA DAR ES SALAAM

Anwani ya Simu:

Simu: 2203156/2203158

Fax: +25522203213

Tovuti: www.dsm.go.tz

Barua pepe : ras@dsm.go.tz



**OFISI YA MKUU WA MKOZA,
3, Barabara ya Rashid Kawawa,
S.L.P. 5429,
12880, DAR ES SALAAM.
Tanzania**

17 Septemba, 2020

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

RC KUNENGE ATEMBELEA MIRADI NA KUTAKA IKAMILIKE KWA WAKATI

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Abubakar Kunenge leo tarehe 17 Septemba, 2020 amefanya ziara ya kukagua miradi iliyopo katika Wilaya za Kinondoni, Ubungo, na Ilala na kutaka miradi hiyo ikamilike kwa wakati uliopangwa.

Awali Mhe. Kunenge alikagua mradi wa ujenzi wa barabara ya Tegeta Nyuki yenyе urefu wa kilometa 1.06 inayosimamiwa na Tarura na kujengwa na kampuni ya CMG Construction iliyopo katika Wilaya ya Kinondoni ambapo alimtaka mkandarasi wa mradi huo kukamilisha ujenzi huo kwa wakati kwani amekua akisusua kumaliza mradi huo licha ya kuongezewa muda.

“Wakandarasi wasipofanya kwa wakati waliopewa wanaongeza kero kwa wananchi, hivyo naagiza mradi huu uwe umekamilika kwa kiwango cha rami na mitaro mizuri ilifikapo Oktoba mwishoni”. Aliagiza RC Kunenge.

Baada ya hapo msafara wa Mhe. Mkuu wa Mkoa ulielekea katika ukaguzi wa ujenzi wa barabara ya Madale kueleke Wazo yenyе urefu wa Kilomita 6 inayogharimu kiasi cha Tshilingi Billioni 9.9 ambapo Mkuu huyo wa Mkoa alifurahishwa na juhudzi za usimamizi na ujenzi wa mradi huo ambapo alisema mkandarasi wa mradi huo yupo ndani ya muda na ujenzi huo unaenda vizuri. Alimtaka mkandarasi huyo pia asibweteke bali aukamilishe mradi huo ndani ya muda uliopangwa.

Aidha, RC Kunenge pia ametembelea na kukagua Mradi wa ujenzi wa Stand Mpya ya mabasi ya kisasa ya Mbezi Louis ambayo ujenzi wake umefika 80% na inagharimu Kiasi cha Shilingi Bilioni 56 ambapo ameonyesha kuridhishwa na hatua ya ujenzi ilipofikia.

Mwisho kabisa RC Kunenge ametembelea ujenzi wa Daraja la Ulongoni A lililopo Kata ya Gongolamboto ambalo ujenzi wake unagharimu Shilingi Bilioni 4.3 na unatarajia kukamilika ifikapo Aprili, 2021 na Ujenzi wa Daraja la Ulongoni B ambapo amewahimiza wakandarasi kuongeza juhudzi kwa kufanya kazi usiku na mchana ili ujenzi ukamilike ndani ya Muda uliopangwa ili kupunguza kero walizokuwa wakizipata wananchi.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Mtaa wa Ulongoni A Bw. Ibrahimu Hamisi alitoa shukrani zake za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuwajali na kuwatengea kiasi hicho cha pesa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo kwani changamoto katika madaraja hayo ni kubwa hasa katika upitaji wa watu, magari, pikipiki na bajaji.

“Mchakato unavyoendelea tunaamini inaweza ikawa faraja kwetu” Alisema Mwenyekiti wa Ulongoni A Bw. Ibrahimu Hamisi.

Imetolewa na:-

Kitengo cha Habari na Uhusiano
OFISI YA MKUU WA MKOA
DAR ES SALAAM